East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 1, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 5, Issue 1, 2022
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# 'Huyu Mtu Hasimami': Uhuishi katika Mazungumzo ya Daktari na Wanaume katika Kliniki ya Afya ya Uzazi, Kenya

*Melvin Atieno Ouma[1], Prof. Jonathan Furaha Chai, PhD[2] & Prof. Catherine Wawasi Kitetu, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Egerton, S. L. P. 536-20115, Njoro, Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Pwani, S. L. P. 195-80108, Kilifi, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0001-5316-9764; Barua pepe ya mawasiliano: melvinouma@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*30 Mei 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Afya Ya Uzazi, Sehemu Za Siri, Uhuishaji, Ujinaishaji, Wanaume.*

**IKISIRI**

Lugha ni kiungo muhimu katika mawasiliano kati ya daktari na mgonjwa. Katika kliniki ya afya ya uzazi, kutaja sehemu za mwili kwa majina yao ni kigezo muhimu katika utoaji na upokeaji wa huduma za afya. Ujinaishaji ni jambo la zamani kama ilivyo ubinadamu. Ujinaishaji wa sehemu za siri ina historia ndefu kutoka karne ya zamani sana. Ujinaishaji wa sehemu hizi ni jambo linalofanyika katika mataifa yote ulimwenguni. Makala haya yanaangazia uhuishi unavyotumiwa na wanaume kama mkakati wa mazungumzo katika kliniki ya afya ya uzazi. Kuafikia hili, makala haya yatashughulikia majina ambayo wanaume wanayapa sehemu zao za siri katika kliniki ya afya ya uzazi. Pia yatafafanua sifa na tabia za kibinadamu zinazopewa sehemu za siri katika mazungumzo ya wanaume na daktari kuhusu matatizo ya afya ya uzazi. Majina kama vile dick, mwanaume, uume, mkuki, chuma na huyu mtu ni baadhi ya majina wanaume walitumia kutaja sehemu zao za siri. Sehemu za siri ya wanaume ilipewa sifa na tabia za kibinadamu kupitia urejeleo kwa ngeli ya A-WA. Matumizi ya ngeli ya A-WA ni idhibati kuwa dhakari ni kama binadamu na wala si sehemu ya mwili ya kawaida kama inavyodhaniwa. Uhuishi ulijitokeza katika mazungumzo kupitia maneno kama vile anakataa, hakubali, hasimami, anajikunja. Semi za wanaume zinaonyesha kuwa dhakari ina uwezo wa kuamuka na kufanya kazi. Dhakari ina uwezo wa kutoa adhabu. Ina uwezo wa kusimama. Ina uwezo wa kuwa imara na ina uwezo wa kuenda. Sehemu za siri za mwanamume zina maisha yake na fahamu zake kando na yule mwanamume anayemiliki sehemu hizo. Kupitia mazungumzo ya daktari na mgonjwa, sehemu za siri (dhakari) ndio sehemu ya mwili inayothaminiwa zaidi miongoni mwa wanaume.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**APA CITATION**

Ouma, M. A., Chai, J. F., & Kitetu, C. W. (2022). 'Huyu Mtu Hasimami': Uhuishi katika Mazungumzo ya Daktari na Wanaume katika Kliniki ya Afya ya Uzazi, Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 131-141. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685.

**CHICAGO CITATION**

Ouma, Melvin Atieno, Jonathan Furaha Chai and Catherine Wawasi Kitetu. 2022. "'Huyu Mtu Hasimami': Uhuishi katika Mazungumzo ya Daktari na Wanaume katika Kliniki ya Afya ya Uzazi, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 131-141. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685.

**HARVARD CITATION**

Ouma, M. A., Chai, J. F., & Kitetu, C. W. (2022) "'Huyu Mtu Hasimami': Uhuishi katika Mazungumzo ya Daktari na Wanaume katika Kliniki ya Afya ya Uzazi, Kenya", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 131-141. doi: 10.37284/jammk.5.1.685.

**IEEE CITATION**

M. A. Ouma, J. F. Chai & C. W. Kitetu "'Huyu Mtu Hasimami': Uhuishi katika Mazungumzo ya Daktari na Wanaume katika Kliniki ya Afya ya Uzazi, Kenya", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 131-141, May. 2022.

**MLA CITATION**

Ouma, Melvin Atieno, Jonathan Furaha Chai & Catherine Wawasi Kitetu. "'Huyu Mtu Hasimami': Uhuishi katika Mazungumzo ya Daktari na Wanaume katika Kliniki ya Afya ya Uzazi, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, May. 2022, pp. 131-141, doi:10.37284/jammk.5.1.685.

## UTANGULIZI

Ujinaishaji ni jambo la zamani kama ilivyo ubinadamu. Ni tabia ya lugha inayopatikana katika jamii zote kwa sababu wanadamu hutumia majina kuwatambulisha na kuwatofautisha watu wake (Aceto, 2002). Jina ni aina ya neno linalotaja au kubainisha viumbe hai, vitu visivyo uhai, mahali, hisia, hali, maarifa na tukio (Msanjila, Kihore & Massamba, 2009). Naye Massamba (2004) anaongezea kuwa jina ni kipengele cha maisha, utambulisho na utamaduni wa binadamu katika jamii mbalimbali. Kazi hii inaangazia majina yaliyotumiwa na wanaume kurejelea dhakari, sehemu ya siri ya mwili, katika kliniki ya afya ya uzazi, wanapozungumzia matatizo ya afya ya uzazi na daktari.

Maana inayoambatanishwa na jina ina jukumu kubwa katika ufafanuzi wa kibinafsi wa mwanadamu (Jayaraman, 2005). Anaongezea kwamba, inaaminika kuwa jina fulani halitumiki tu kama utambulisho wa kijamii lakini pia huathiri nyanja kadhaa za maisha ya mwanadamu. Majina sio tu maneno ya kidhahania yaliyowekwa kwa muda usiojulikana, bali ni zaidi ya kitambulisho ambayo yamejaa maana na ishara (Olatunji na wenzake, 2015; Udechukwu & Nnyigide, 2016). Kwa misingi ya maelezo haya, jina linaweza kueleza sifa za mtu au kitu na hubeba maana maalumu kama ilivyo katika majina yaliyotumiwa na wanaume kurejelea dhakari walipotafuta huduma za afya ya uzazi hospitalini.

Dhakari ni sehemu ya uchi wa mbele wa mwanamume. Ni kiungo kinachotumiwa katika kushiriki ngono na kwa kawaida pia hutumiwa kama njia ambayo mkojo hupitia ili kutoka mwilini. Uwezo wa dhakari kuwa ngumu, kubwa na yenye nguvu wakati wa usimikaji ndio inayoipa uwezo wa kutekeleza kazi yake. Kutokana na hili, dhakari kama walivyo wanadamu, ina umuhimu na hivyo kupewa majina kama binadamu. Ujinaishaji wa dhakari una historia ndefu kutoka karne ya zamani sana. Majina kama vile *pin* (1460), *silent flute* (1720), *shaft of delight* (1772), *dick* (1836), *hot dog* (1925), *ambassador* (1927), *candystick* (1928) ni mifano tu ya baadhi ya majina ya dhakari yaliyotumiwa hapo awali. Hata hivyo haijulikani ni lini hasa ambapo binadamu alianza kuunda majina mbalimbali ya kiungo hiki.

Ujinaishaji wa kiungo hiki ni jambo linalofanyika katika mataifa yote ulimwenguni. Baadhi ya majina yanayotumiwa kote ulimwenguni ni kama vile majina ya nyoka: *anaconda* na *python*; majina ya watu kama vile: *Willy*, *Johnson*, *Jimmy* na *Johny*; majina ya chakula kama vile: *banana*, *lollipop* na *sausage*; majina ya vifaa vigumu kama vile: *hammer*, *baseball bat*, *knob*, *firehose* na *rod;* majina ya miungu kama vile *Zeus*; majina ya mazimwi kama vile: *one-eyed monster*; majina ya shujaa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685

kama vile: *Hercules*; majina mengine kama vile *dick, cock, big boy, big guy, member, pecker* na *little man.* Majina haya ni mengi sana hayawezi kuorodheshwa yote. Nchini Kenya, baadhi ya majina yanayojulikana na kutumika kitaifa ni kama vile *queen B machine gun, tarimbo, lolo, mjulubeng/mjulus, member, rungu, mboko haram, chuma ya doshi* na *mti*. Sifa kuu inayounganisha majina haya ni kuwa ni majina yanayorejelea sehemu za siri ya mwanamume (Cornog, 1986), mahususi, dhakari. Cornog anaongezea kuwa, haya ni majina, wala si istilahi. Kwa kawaida, binadamu hawatafuti na kupea sehemu za mwili kama vile macho, mikono, mabega majina. Hata hivyo, baadhi ya watu hupea sehemu za siri majina, hasa dhakari, miongoni mwa wanaume.

Majina yanayopewa dhakari ni ishara kuwa wanaume wanachukulia dhakari zao kama 'watu' tofauti na wao, na walio na maisha ya pekee (Cameron, 1992). Anaongezea kuwa, ujinaishaji wa dhakari miongoni mwa wanaume unaonyesha uhusiano wa kibinafsi na wa kipekee ambao upo kati ya wanaume na dhakari zao. Ujinaishaji wa dhakari ni kama haijatiliwa maanani na watafiti ulimwenguni kama tabia ya kipekee ya ngono (Cornog, 1986). Inasahaulika kuwa Cornog asema, katika jamii zote, ni sehemu za siri tu ndizo zinazopewa majina ya kipekee. Kazi hii inaangazia ujinaishaji na urejeleo wa dhakari na wanaume, wanapozungumzia matatizo ya afya ya uzazi.

Kazi hii pia inaelezea jinsi dhakari inavyopewa sifa na tabia za binadamu (uhuishi) katika kliniki za afya ya uzazi nchini Kenya.

## UJINAISHAJI

Majina yamegawanyika katika makundi kama vile majina jumuishi, majina mahususi na majina makundi (Msanjila, Kihore & Massamba, 2009). Jina huwa na nguvu na athari kwa mwenye nalo na mengi ya majina maana yake huwa na kitu au dhana ambayo hukumbusha jamii matukio mbalimbali ya kijamii (Resani, 2016). Majina huwa na historia ndefu kwani mengine huwa ni ya wazazi wa anayehusika, jamaa wa karibu ama yameshawahi kutumiwa na watu mashuhuri kwa mfano wanamuziki, wanasiasa au jamii teule (Musyimi, 2011).

Majina si maneno ya kufikirika tu yaliyowekwa kwa muda usiojulikana, majina ni zaidi ya vibandiko ambayo yamejaa maana na ishara (Olatunji, Issah, Yusuf, Mohammed & Sulaiman, 2015). Wanadamu pekee ndio wenye kipawa cha kutaja watu au vitu majina maalum. Muundo wa majina unaotumiwa na wanadamu ni wa kipekee kwa spishi ya wanadamu tu (Yusuf, Olatunji & Issah, 2014). Ingawa matukio yote yanayojulikana na yasiyojulikana yana majina, jina la mwanadamu lina umuhimu zaidi wa kijamii kuliko majina ya vitu (Olatunji na wenzake, 2015). Jina ni suala muhimu ambalo huathiriwa na sababu nyingi na pia huathiri ukweli wa kijamii. Dhakari ni sehemu ya mwili inayoashiria nguvu za jinsia ya kiume kutokana na uwezo wake wa kusimika na kutunga mwanamke uja uzito. Ni kutokana na nguvu hizi, ndiposa sehemu hii ya mwili ina majina mbalimbali kote ulimwenguni.

Jina ni alama ya utambulisho wa mtu yeyote na kitu chochote ambacho hutofautisha mtu mmoja na mwingine kati ya watu wengine (Udechukwu & Nnyigide, 2016). Iwe ni jina la utani au majina ya kiume, mradi tu inamfanya mtu au kitu kuonekana kuwa tofauti na watu wengine au kitu kingine. Majina yanayopewa dhakari, yanafanya sehemu hii ya mwili kuonekana kuwa tofauti na sehemu nyingine ya mwili. Hii ni kwa sababu hakuna sehemu nyingine ya mwili inayotafutiwa majina tofauti. Kwa mfano, mikono, miguu, tumbo ni sehemu za mwili zinazorejelewa na majina ya kibayolojia. Hata hivyo, sehemu za siri tu ndizo zinapewa majina tofauti na yale majina ya kibayolojia. Pia majina yanayopewa sehemu za siri ni majina ambayo yanapotajwa tu, wasikilizaji huweza kubaini kinachozungumziwa. Ni majina yanayojisimamia na kujitambulisha kivyao.

### Ujinaishaji wa Sehemu za Mwili za Wanaume

Majina ambayo wanaume huwapa dhakari zao yanaweza kuwekwa katika kategoria tatu (Cameron, 1992). Kategoria ya kwanza ni majina ya hadhi na mamlaka ambayo ni pamoja na: *his excellency, your majesty, the chief, the commissioner, the mayor* na *the judge*. Haya ni majina yenye hadhi na utukufu katika jamii. Watu wenye majina haya hupewa heshima ya kipekee na wanajamii. Katika kategoria hii pia kuna majina ya mamlaka kama vile *scepter, rod of lordship, excalibur* na *hammer of the gods.*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685

Misingi ya majina haya ipo katika kuhusishwa na watu wenye nguvu na mamlaka katika jamii. Majina haya yanaonyesha kuwa wanaume wanatawaliwa na dhakari zao. Kwamba dhakari ni kama mwanamume halisi, pasi na kuhusishwa na mwenye kuibeba.

Kategoria ya pili kulingana na Cameron ni majina ya mashujaa wanaopatikana katika visasili, ngano za mashujaa, kwenye runinga na hata vitabu vya vichekesho. Kwa mfano *Ghenghis Khan* na *Cyclops* ambapo dhakari inarejelewa kama mtu mwenye jicho moja, mwenye kimo kirefu na nene/kubwa sana. *The Hulk, the Lone Ranger* na *the Purple Avenger* ambao ni mashujaa wanaopatikana katika vitabu na filamu ya *Avengers*; *Mac the knife* na *Kojak* ambazo zinachukulia dhakari kama silaha. Kategoria ya tatu ni tofauti, kwani ina majina yanayoonyesha urafiki, uhusiano wa kindani na mapenzi ya dhakari. Majina haya ni kama vile *Dick, Peter, Percy, John Thomas, Johnson* na *Mr. Happy*.

Majina mengine kama anavyoeleza Cameron ni kama vile majina ya wanyama: wanyama wa kiuhalisia ajabu *King Kong, Simba, King of the Jungle, The Dragon* na *Cujo*. Majina ya nyoka *snake, one-eyed trouser snake, python, cobra* na *anaconda.* Majina ya wanyama wengine ni kama vile *cock, hog, weasel, hairy hound of hedonism* na *beast of burden*. Majina mengine ni ya vifaa kama vile *pole, pipe, gardenhose, screwdriver, drill, jack hammer, chisel, lawnmower* na *hedge trimmer*. Majina haya ya vifaa yanaibua hisia ya dhakari iliyosimika inavyokaa na kufanya kazi. Kwa wanaochukulia tendo la ngono kama vita basi majina ya zana za vita zinazotumiwa kurejelea dhakari ni: *bunduki, mikuki, visu* na *kombora*.

Wazulufu wana majina mbalimbali ya kurejelea dhakari (Gacheiya, 2018). Gacheiya aligundua kuwa majina kama vile *zigo,* majina ya chakula kama vile *muwa* na *banana*, majina ya bunduki *pistol* na majina ya vifaa kama vile *nyundo, booster, transformer, bazooka, fimbo ya nyayo, chuma, shaft na kalamu* yalitumiwa na wazulufu wa kike na kiume nchini Kenya, kuita dhakari. Maumbo na dhima ya majina ya vifaa hivi yanaashiria nguvu na uwezo wa dhakari. Hii ni kwa sababu vifaa hivi kwa kawaida ni nyoofu na ngumu, sawia na dhakari iliyosimika.

Majina inayopewa dhakari na wanaume wenyewe yanaonyesha nguvu za dhakari (Sanders, 1978). Sanders anaongezea kuwa wanaume wanazipa dhakari zao majina ya kipekee, ya kuonyesha uhusiano wa kindani na nguvu kinyume na wanawake wanavyoshindwa kuzipa sehemu zao za siri majina. Dhakari lazima iwe na uwezo wa kutenda, kuhodhi na kujilipizia kisasi katika mwili wa jinsia ya kike. Ni ishara ya nguvu na mamlaka ambayo lazima sote tuiinamie (Cameron, 1992). Tamaa ya dhakari ya kinyama haiwezi kudhibitiwa kwa sababu dhakari ina maisha yake pekee yake. Dhakari ni muhimu, ni muhimu ya kutosha, hivi kwamba inapewa takriban majina 144 tofauti (Cameron, 1992).

**Uhuishi wa Sehemu za Mwili za Wanaume**

Uhuishi ni mbinu ya lugha ambapo vitu visivyo na uhai hupewa sifa na tabia za binadamu, hivyo kupewa uhai. Mbinu hii pia hujulikana kama tashihisi. Sababu ya kuuhuisha dhakari katika mazungumzo inatokana na haja ya kuonyesha kuwa dhakari ina nafsi yake, hulka yake na maisha yake tofauti na yule mwanamume mwenye hiyo dhakari (Cornog, 1986). Kwa hivyo, sifa na tabia zinazopewa dhakari pamoja na majina yanayotumiwa kuirejelea si istilahi bali ni majina. Kwa kawaida, sehemu zote za mwili hazipewi majina mahususi isipokuwa sehemu za siri.

Uhuishi wa sehemu za siri miongoni mwa wanaume inatokana na haja ya kutumia tasfida (Sanders & Robinson, 1979). Hata hivyo, Cornog (1986) anapinga madai haya ya Sanders na Robinson na kusema kuwa uhuishi wa sehemu za siri miongoni mwa wanaume unatokana na haja ya kuimarisha uhusiano wa kihisia baina ya mwanamume na dhakari yake. Hii ni kwa sababu mara nyingi mtu na dhakari yake huchukuliwa kuwa watu wawili wenye hisia tofauti.

Maumbile ya dhakari kwa nje inavyoonekana inaunda mgawanyiko wa ndani-nje wa mwili wa mwanaume ambao kwa kawaida hauonekani katika viungo vya uzazi vya wanawake (Potts, 2001). Hivyo, uhusiano wa mwanaume na dhakari yake hufuata maumbile haya ya ndani-nje. Dhakari huhusishwa na hali ya nje ya mwili hivi kwamba ina fahamu zake yenyewe ambazo ni tofauti na akili ya mwanamume ambaye dhakari hiyo imeshikamana

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685

nayo. Hii ndiyo hali inayoangaliwa katika kazi hii. Kwani kutokana na deta, inabainika kuwa kulingana na wanaume, kuna tofauti kati ya mwanamume na dhakari yake. Pia inaonekana kuna uhusiano wa kipekee kati ya mwanamume na dhakari yake.

Dhakari mara kwa mara hujulikana kama mtu mwenye fahamu zake. Inachukua sifa za kibinadamu ambazo huifanya kuonekana kuwa isiyoweza kudhibitiwa na isiyoweza kutii mwili ambao imeshikamana nao (Potts, 2000). Kwa misingi ya maelezo haya, kuna uwezekano kuwa kuja kwa wanaume katika kliniki ya uzazi kutafuta huduma za afya ya uzazi, unatokana na ukosefu wa 'kuelewana' kwa mwili wa mwanamume husika na dhakari yake. Ndio maana kwa mfano, ingawa mwanamume anaweza kuwa na hamu ya kushiriki ngono, anakosa uwezo wa kusimika. Kwa sababu ya dhana kuwa mwanamume na dhakari yake ni watu wawili tofauti, kila mtu na akili zake.

## MISINGI YA NADHARIA

Kurunzi ya kazi hii ni nadharia ya ujinaishaji. Ni nadharia ya maana katika semantiki inayojaribu kuonyesha uhusiano baina ya jina na kiwakilishi chake. Nadharia ya ujinaishaji kwa kuangazia mkabala wa maelezo (*descriptive approach*), unaoshikilia kuwa majina na maelezo (*descriptions*) yanafungamanishwa pamoja kama mahusiano ya visawe, uliasisiwa na Frege na Russell.

Mkabala wa maelezo ya majina unaeleza kuwa kila jina lina thamani ya kisemantiki ya maelezo dhabiti (*definite descriptions*) (Al-Dilaimy & Thabiti, 2017). Yaani, maana ya majina inafanana na sifa zinazobebwa na maelezo. Mantiki ya majina inabeba maelezo ambayo mzungumzaji anatumia kuhusisha maelezo hayo na jina husika (Frege, 1892). Hivyo, kwa misingi ya maelezo haya, majina yanayopewa sehemu za siri za miili na wanaume katika kliniki za afya ya uzazi yamebeba maelezo ndani yazo. Majina hayo ni maneno moja moja ambayo huenda yakachukuliwa kuwa maneno tu ya kawaida. Hata hivyo kama anavyonukuliwa Russell (1905) na akina Al-Dilaimy na Thabiti (2017), jina hata liwe fupi kiasi gani huwa ni ufupisho wa maelezo ya kinachorejelewa na jina hilo. Majina yaliyopewa dhakari na wanaume katika kliniki za afya ya uzazi ni maneno moja moja ya watu, wanyama na hata vifaa. Bila kufikiria zaidi, majina hayo yalionekana kuwa majina ya kawaida. Hata hivyo, katika majina hayo, ndani kuna maelezo zaidi, ambayo kwa kupiga msasa zaidi, maelezo yazo yamebebwa kwenye sifa na tabia za binadamu zinazopewa dhakari.

Jina hubeba maelezo yake ambayo huwa inategemea muktadha wa mazungumzo (Allan, 2001). Kwa kujua au kutojua, majina yaliyopewa dhakari yalisheheni sifa na tabia za binadamu. Iwapo muktadha wa mazungumzo haya ungetupiliwa mbali, basi msikilizaji anaweza kufikiria kuwa anayezungumziwa ni binadamu mwingine mwenye uhai, uwezo wa kutenda na mwenye razini.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ni wa kithamano mkabala wa uchanganuzi usemi. Utafiti wa kithamano husaidia kuelewa na kueleza tajriba ya watu na jambo mahususi kuhusu watu wanaotafitiwa (Howlett na wenzake, 2014). Utafiti wa kithamano ni mchakato wa kuelewa maswala ya jamii na matatizo ya binadamu (Creswell, 1998). Uchanganuzi usemi kama mkabala wa utafiti wa kithamano, huangalia muundo maalum wa mazungumzo na mwingiliano kati ya wasemaji wawili au zaidi kuelewa jinsi maana za pamoja zinajengwa kijamii (Guest na wenzake, 2013). Guest na wenzake wanaongezea kuwa mkabala huu hutafiti lugha katika muktadha asilia kinyume na matini inayotokana na muktadha uliobuniwa. Utafiti ulifanyiwa katika hospitali ya umma mjini Nakuru katika jimbo la Nakuru, nchini Kenya, ambayo ilichaguliwa kimakusudi. Idhini zote zinazohitajika ili kukusanya deta ya aina hii zilipatikana kulingana na sheria za utafiti nchini Kenya.

Wanaume wapatao 100 waliotembelea kituo cha afya kutafuta huduma za afya ya uzazi katika kipindi cha miezi mitatu walishirikishwa. Wanaume hao walishirikishwa kwa hiari. Uchunguzi-shiriki ulitumiwa kukusanya lugha waliyotumia wanaume kuelezea hali zao za kiafya katika mfumo wa uzazi walipotafuta huduma za afya ya uzazi. Kinasa sauti kilitumiwa kurekodi mazungumzo kati ya daktari na mgonjwa. Unukuzi wa deta ulifanywa kwa kuambatanisha kila mzungumzaji na usemi wake. Majina ya washiriki na daktari yaliyotumiwa si majina yao halisi. Majina hayo yamebadilishwa,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685

huku yakihifadhi asili ya mzungumzaji kikabila na kiutamaduni. Nambari katika mazungumzo inasimamia zamu ya uzungumzaji.

## MATOKEO

Matokeo ya kazi hii yametolewa kwa misingi ya madhumuni yaliyoongoza kazi hii. Kutokana na mazungumzo ya daktari na wagonjwa (wanaume) katika kliniki ya afya ya uzazi, wanaume wana uhusiano wa kipekee na dhakari zao. Dhakari zinaporejelewa, zinapewa heshima ya viumbe vyenye uhai. Kwanza zinazungumziwa kwa ngeli ya A-WA kuonyesha ni viumbe vyenye uhai. Pili dhakari ni kama binadamu bali si sehemu tu ya mwili kama ambavyo imefikiriwa kwa kawaida. Madai haya na matokeo yanadhibitishwa na kuonyeshwa ifuatavyo:

### Majina ya Sehemu za Mwili za Wanaume katika Kliniki ya Afya ya Uzazi

Kliniki ya afya ya uzazi inatoa huduma za matatizo yanayoathiri mfumo wa uzazi. Wanaume walitembelea kliniki hii kupata suluhisho ya matatizo mbalimbali kama vile matatizo ya dhakari, magonjwa ya zinaa, matatizo ya korodani na maambukizi katika njia ya mkojo. Ili kuweza kupata huduma ya matatizo haya, lazima mgonjwa aeleze anavyohisi. Katika kufanya hivyo, analazimika kutaja sehemu mbalimbali za mwili ambazo katika muktadha huu zilihusisha sehemu za siri.

Sehemu za siri za wanaume zimegawika kuwili: kuna dhakari na mfuko wa pumbu. Dhakari ndio sehemu ambayo hutumiwa kupitisha mkojo kutoka mwilini. Pia ndio sehemu ambayo husimika na hutumiwa wakati wa kushiriki ngono. Ndani ya mfuko wa pumbu kuna pumbu/korodani ambazo huwa zimebeba na kuhifadhi manii. Ili kurejelea sehemu hizi, majina tofauti tofauti yalitumiwa na wanaume wa utamaduni tofauti tofauti. Majina yafuatayo yalitumiwa na wanaume kuita dhakari.

**Jedwali 1: Ujinaishaji wa dhakari**

| | Jina | Msemaji |
|---|---|---|
| 1 | Huyu mtu | Mutua, miaka 58 |
| 2 | Uume wangu | Kinyanjui, miaka 54 |
| 3 | Kiungo hiki changu | Mutuku, miaka 52 |
| 4 | Mwanaume | Mwaura, miaka 48 |
| 5 | Kidole | Kiptum miaka 44 |
| 6 | Mkuki, chuma | Korir, miaka 35 |
| 7 | Dick | Wanyonyi, miaka 32 |
| 8 | Phallus yangu | Otieno, miaka 27 |
| 9 | Penis | Kefa, miaka 26 , Okinyi, miaka 17 |
| 10 | Tarimbo haichapi | Luvisi, miaka 26 |
| 11 | Kitu ya kukojoa | Ondiek, miaka 23 |

Jedwali hili linaonyesha kuwa kila mwanamume alikuwa na njia yake mwenyewe ya kutaja dhakari. Matumizi ya lugha ya Kiingereza *penis* na *phallus* yanatumiwa na vijana ni uteuzi wa kimakusudi. Yanaonyesha hadhi ya watu hawa katika jamii, wana kiwango fulani cha kisomo ndio maana wanaweza kutumia lugha ya Kiingereza. Kutumia lugha ya Kiingereza katika muktadha huu kulionekana kuwa na wepesi fulani ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili au lugha za kwanza.

*Tarimbo* ni kifaa kinene cha chuma kilichonyooka ambacho hutumiwa kuchimba shimo au ardhi ngumu. Nchini Kenya, neno *tarimbo* limepoteza maana asilia ya chuma na kupata maana mpya: dhakari. Neno hili kulitaja linahitaji uhakika wa muktadha. Neno tarimbo lilienezwa na kusambazwa kumaanisha dhakari nchini Kenya Novemba, mwaka wa 2019 wakati ambao kikundi cha Ethic Entertainment walitoa wimbo ulioitwa *Tarimbo*. Katika kiitikio cha wimbo huo kuna mstari “mi hupenda chapa na *tarimbo*”. Kuanzia kipindi hicho,

neno hili likapokelewa kwa maana hiyo ya dhakari ilhali kitendo cha "kuchapa" kikapokelewa kama kushiriki ngono.

*Mkuki* na *chuma* ni vifaa ambavyo vinatumiwa katika vita, ni vifaa vigumu visivyoweza kuvunjika kwa urahisi. Dhakari imepewa majina haya kwa sababu ya ugumu wake inaposimika. Mkuki na chuma pia ni vifaa nyoofu kama ilivyo dhakari wakati imesimika tayari kwa "vita". Majina haya yanaashiria kuwa tendo la kushiriki ngono ni vita na hivyo zana faafu kama vile *mkuki* huhitajika.

*Mwanaume* na *huyu mtu* ni majina yanayotumiwa kuita dhakari. Washiriki hawa wanapotumia majina haya, mazungumzo hayo yanatokea ni kama wanazungumzia watu wengine wa kando ambao wana nguvu fulani. Mazungumzo haya yanatokea katika muktadha wa kliniki ya afya ya uzazi ndio maana ni rahisi kugundua kuwa wanachorejelea hapa ni dhakari.

*Dick* ni mojawapo ya majina ya zamani sana yaliyowahi kutumiwa na jamii zote ulimwenguni. Jina hili kulingana na Cameron (1992) huonyesha urafiki wa kindani na hata mapenzi. Jina hili linaonyesha dhakari kama 'mtu' mwenye mapenzi wala si vita au mamlaka.

**Uhuishi katika Mazungumzo Yanayotokea katika Kliniki ya Afya ya Uzazi**

Wanaume walipotembelea kliniki ya afya ya uzazi, walijieleza kwa njia mbalimbali. Mojawapo ya njia hizo, ilikuwa ni uhuishi. Dhakari, sehemu ya siri ya wanaume ilipewa sifa na tabia za binadamu. Uhuishi ulitumiwa kama mkakati wa kujieleza, daktari na wagonjwa wa kiume walipozungumzia matatizo ya afya ya uzazi. Uhuishaji ulijitokeza katika mazungumzo kama ifuatavyo:

**Mfano 1:**

Saa 1:21 mchana - Mgonjwa 7: Kioko , miaka 53

*23 Kioko: Daktari hiyo shida ingine ni sina hamu ya tendo la ndoa.*

*24 Dkt. Chebet: Hiyo imeletwa na hii pressure kuwa juu. Kwa muda gani?*

*25 Kioko: Miezi saba. Hata* ***nikisikia napata hamu hakubali kusimama*** *(anajigusagusa kichwa).* ***Anakataa kabisa kuamuka****.*

*26 Dkt. Chebet: Kwa sababu pressure iko juu blood supply hapo si enough kwa sababu vessels zimekuwa very thin* (Ijumaa, 14-01-2022)

Mshiriki huyu anaipa dhakari yake uwezo wa *kukubali* na *kusimama*. Ni kama dhakari ina fikra zake hivi kwamba anaweza kushawishiwa *kukubali* au *kukataa*. Kutokana na mazungumzo haya, ni kana kwamba dhakari yake *ameshawishiwa* lakini amekataa *kukubali* kushawishika *kusimama*, yaani kusimika.

**Mfano 2:**

Saa 3:14 mchana Mgonjwa 11: Mutua, miaka 58

*13 Dkt. Kirui: Nini ilifanyika?*

*14 Mutua: Yaani* ***saa hii huyu mtu hasimami****.*

*15 Dkt. Kirui: Hata ukikutana na mke?*

*16 Mutua: Mmmm... Si mke, huyo ni wa kushikilia tu.*

*17 Dkt Kirui: Kama girlfriend?*

*29 Dkt Kirui: So you were sexually active halafu all of a sudden ikaanza kuisha?*

*30 Mutua: Eeeh.* ***Nilikuwa tu sawa nikashtukia tu sasa hasimami*** (Jumatatu, 17-01-2022).

Mshiriki anaipa dhakari yake tabia za kibinadamu. Kwanza bila kusita anasisitiza kuwa dhakari yake imekosa uwezo wa kusimika. Katika kufanya hivyo anairejelea dhakari yake kama binadamu mwingine; *huyu mtu*. Kando na kumrejelea kama mwanadamu mwenzake anampa uwezo wa kusimama ambao unaeleweka unarejelea kusimika.

**Mfano 3:**

Saa 3:22 mchana Mgonjwa 17: Kimani miaka 54

*(Anasimama na kuanza kuondoka. Anafika mlangoni, anaugusa lakini hafungui mlango. Anarejea tena.)*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685

*46 Kimani: lakini sasa wacha niwaulize* ***mimi nikitaka kufanya hii kazi usiku anakataa kuamuka****.*

*47 Dkt. Kirui: Hiyo sasa ni tofauti. Prostrate haiwezi fanya ukawa na...*

*48 Kimani:* ***Kutoamuka***

*49 Dkt. Kirui: kutoamuka inasababishwa na emotional status, kama uko na mafikira mingi*(Jumatano, 19-01-2022).

*Kazi* inayozungumziwa katika muktadha huu ni tendo la ndoa. Kifaa (dhakari iliyosimika) kinachohitajika kufanya *kazi* hii hakisalimu amri. Dhakari yenyewe imekwisha jizungumzia na kujishawishi kuhusu kufanya kazi hivyo *anakataa kuamka*. Ni kana kwamba amelala na hana mpango wa kutoka usingizini.

**Mfano 4:**

Saa 9:08 Mgonjwa 23: Kinyanjui miaka 54

*3 Dkt. Chebet: Kinyanjui uko na shida gani?*

*4 Kinyanjui: Niko na shida ya …* ***na uume wangu****.*

*5 Dkt. Chebet: Mmmmh.*

*6 Kinyanjui: sasa hii uume wangu …* ***kwanza akisimama nasikia uchungu sana****.*

*7 Dkt. Chebet: Mmmmh.*

*8 Kinyanjui:* ***Halafu akisimama*** *(kwa kutumia kidole cha pili cha mkono wa kulia kama dhakari na kidole cha pili cha mkono wa kushoto anafanya kama kusugua kidole cha pili cha mkono wa kulia)* ***hasimami straight vile inafaa****.*

*9 Dkt Chebet: Mmmmh.*

*10 Kinyanjui:* ***Anasimama hivi*** *(anatumia kidole cha pili kuonyesha kupinda)* ***kama amejikunja****.*

*11 Dkt. Chebet: Hujawahi tumia dawa yoyote?*

*12 Kinyanjui: Dawa kama gani?*

*13 Dkt. Chebet: Dawa ya sukari hivi?*

*14 Kinyanjui: hapana* (Jumatatu, 24-01-2022).

Kinyanjui anapozungumzia *uume* wake moja kwa moja inaeleweka kuwa anazungumzia dhakari yake. Hata hivyo maelezo anayotoa baadaye yanaonyesha kuwa huu *uume* ni kama binadamu. Ni kama binadamu kwa sababu *akisimama* kuna uchungu mwingi. Hali hii anayojipata Kinyanjui ni ile ya uchungu wakati wa kusimika. Dhakari ya Kinyanjui imepewa uwezo wa *kusimama*, ingawa haisimami na *kujikunja* kama anavyojikunja binadamu anapolala kwa mfano.

**Mfano 5:**

Saa 3:22 mchana Mgonjwa 43: Kefa miaka 26

*1 Dkt. Kirui: Niambie?*

*2 Kefa: Nasikia uchungu hapa chini hapa chini ya tumbo.*

*3 Dkt. Kirui: Mmmmh.*

*4 Kefa:* ***Naskia uchungu hapa kwa testes****.*

*5 Dkt. Kirui: Mmmmh.*

*6 Kefa:* ***Halafu sasa penis hasimami vile alikuwa anasimama kitambo****.*

*7 Dkt. Kirui: Na nini ingine?*

*8 Kefa: Mmmmh?*

*9 Dkt. Kirui: Na nini ingine?*

*10 Kefa: Halafu feelings… sina feelings ya sex* (Ijumaa, 4-02-2022).

Ingawa Kefa anatumia *penis*, jina la Kiingereza, hiyo *penis* imepewa uwezo wa kusimama ingawa *hasimami* kama alivyokuwa *anasimama* hapo awali.

**Mfano 6:**

Saa 10:38 asubuhi Mgonjwa 54: Nyamori, miaka 43 Abagusii

*13 Dkt. Chebet: Nini imekuwa fupi?*

*14 Nyamori: Yaani tukianza ninaenda dakika kidogo.*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685

*(kimya sekunde 43)*

*15 Nyamori: na mimi nimeona siku hizi inakuja haraka. **Anaingia kidogo tu moja mbili tatu inamwagika**.*

*16 Dkt. Chebet: Unarelease haraka?*

*17 Nyamori: Eeh, hiyo.*

*18 Dkt. Chebet: Na kitambo ilikuwa sawa?*

*19 Nyamori: Kitambo hata **dakika ishirini ako imara kabisa**. Baada tu ya ile ya kwanza unajua lazima ikuje haraka baada ya dakika kumi hivi. **Lakini safari ya pili ya tatu na hizo zingine alikuwa anaenda hata dakika ishirini**.*

*20 Dkt. Chebet: Uko na miaka ngapi?* (Alhamisi, 17-02-2022)

Dhakari ya Nyamori imepewa tabia na uwezo wa *kuingia, kuwa imara kabisa na* hata *kuenda safari*. Hizi ni sifa ambazo binadamu anazo. Kwa sababu kuingia na kuenda kunahitaji miguu ikisaidiwa na sehemu nyingine za mwili kama vile macho inayotazama ni wapi mtu anaenda au kuingia. Ingawa dhakari haina miguu wala macho, tabia hizi zimenasibishwa na hali ya dhakari wakati wa kushiriki ngono.

**Mfano 7:**

Saa 3:51 mchana Mgonjwa 52: Luvisi miaka 26

*1 Luvisi: Niaje mzito?*

*2 Dkt. Wanjala: poa.*

*3 Luvisi: Mzito nimecome juu ya ngori.*

*4 Dkt. Wanjala: Ngori ni gani?*

*5 Luvisi: **Kukula dem imekuwa noma**.*

*6 Dkt. Wanjala: Imekuwa noma?*

*8 Dkt. Wanjala: Hebu nishow hiyo noma niaje!*

*9 Luvisi: **Tarimbo haichapi**.*

*10 Dkt. Wanjala: Tangu lini?*

*11 Luvisi: Miezi kadhaa.* (Alhamisi, 17-02-2022)

Kwa mshiriki huyu, Luvisi *kukula dem* haiwezekani kwa kuwa *imekuwa noma*. Inachukuliwa kuwa dhakari ina 'mdomo' na 'meno' sehemu muhimu zinazohusika na ulaji. Katika muktadha huu, kule *kukula* kunaashiria kushiriki ngono ambapo *dem* (msichana) ndio chakula na dhakari ndio mlaji.

**Mfano 8:**

Saa 9:07 asubuhi Mgonjwa 53: Mwaura miaka 48 na mkewe

*35 Mkewe Mwaura: Mimi kwanza nataka apimwe nijue si dawa anafanya kumeza halafu anakuja kunifanya kama wazimu (anaongea lugha ya kwanza) mimi hutaniumiza.*

*37 Dkt. Chebet: Halafu mzee nataka uende lab ufanyiwe hii test. Halafu nitakuandikia dawa mzuri utameza na itawasaidia nyinyi wote. Mkionana hakuna mtu atasikia uchungu na mpunguze hasira.*

*38 Mwaura: Ni sawa daktari. Lakini huyu ajue kuniita kehe ilikuwa makosa kubwa sana. (Akijiguza sehemu ya siri.) **Huyu ni mwanaume kamili na atakucharaza upende usipende**.* (Jumatano, 2-03-2022*)*

Mahusiano ya Mwaura na mkewe yana tatizo kwa sababu tendo la ndoa halina raha tena. Mkewe Mwaura anahisi uchungu na kutokana na tathmini ya daktari, hana tatizo lolote. Mkewe Mwaura anasisitiza kuwa Mwaura anameza dawa za kusisimua misuli, inayofanya dhakari ya mumewe kusimika na kuwa ngumu zaidi ya kawaida. Kwa sababu ya matusi na kejeli ya hapo awali kati ya wanandoa hawa, Mwaura anamhakikishia mkewe kuwa *huyu* (dhakari) ni *mwanaume kamili*. Anapozungumzia *huyu mwanaume*, kauli yake inajitokeza ni kama dhakari ni binadamu mwingine kando na wao, na yuko hapo karibu na ni mmoja wa washiriki katika mazungumzo haya, ingawa sivyo. Dhakari imepewa uhai, ubinadamu na jinsia ya kiume.

**MJADALA**

Ujinaishaji wa dhakari ni jambo la kawaida kama vile kupea milima, vitu na mahali majina. Hata hivyo, majina yanayopewa dhakari yana maana mahususi na yanaonyesha uhusiano uliopo kati ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685

dhakari na wanaomiliki dhakari. Mazungumzo ya daktari na wagonjwa wanaume yanaonyesha kuwa dhakari ni kiungo muhimu sana cha mwili kwa wanaume. Kando na inavyofikiriwa, sehemu hii ya mwili si kama sehemu yoyote ile, sehemu hii ni kama mwanadamu na ina uhai. Ni sehemu ya mwili inayothaminiwa zaidi miongoni mwa wanaume. Umuhimu wa kiungo hiki na ubinadamu wake unaonekana kwa kurejelewa kwa Ngeli ya A-WA: *Anakataa, hakubali*. Matumizi ya ngeli ya A-WA ni idhibati kuwa dhakari ni kama binadamu na wala si sehemu ya mwili ya kawaida kama inavyodhaniwa.

Semi za wanaume zinaonyesha kuwa dhakari ina uwezo wa kuamuka na kufanya kazi. Dhakari ina uwezo wa kutoa adhabu *atakucharaza upende usipende*. Ina uwezo wa kusimama ingawa haina miguu. Ina uwezo wa kuwa imara na ina uwezo wa kuenda. Kwa mujibu wa maelezo ya Cameron (1992), dhakari ni kiungo cha nguvu na mamlaka katika jamii na sisi sote lazima tuiinamie. Kuwepo kwa mwanamke katika mazungumzo ya daktari, mwanamume na mkewe ni ishara kuwa nguvu za dhakari si chache na kiungo hiki ni kama zana za kupigana katika vita (ngono). Thamani inayopewa dhakari inatokana na ukweli kuwa uwezo wa dhakari kusimika, kushiriki ngono na hata kumtunga mwanamke mimba ndio fasili ya kuwa mwanamume (Ouma, 2018; Izugbara, 2005). Misingi ya ubabedume ipo katika uwepo na uwezo wa dhakari.

Uhuishi wa dhakari miongoni mwa wanaume unaonyesha uhusiano wa kibinafsi na wa kindani uliopo baina ya wanaume na dhakari zao. Uhuishi huu unadhibitisha kauli ya Cornog (1986) kuwa uhuishi wa sehemu za siri miongoni mwa wanaume unatokana na haja ya kutaka kuimarisha uhusiano wa kihisia baina ya mwanamume na dhakari yake. Dhakari ina akili na fahamu zake na ndio maana ina uwezo wa *kukataa* amri ya kusimika inayotoka kwa mwili ambao umeshikamana nayo. Tamaa ya dhakari ya kinyama haiwezi kudhibitiwa kwa sababu dhakari ina maisha yake pekee yake (Cameron, 1992) na fahamu zake kando na mwanaume ambaye dhakari hiyo imeshikamana naye.

## HITIMISHO

Kazi hii imefaulu kuonyesha dhakari ni sehemu ya mwili iliyo muhimu sana miongoni mwa wanaume. Umuhimu huu unadhibitishwa na uhai, ubinadamu na akili ambazo dhakari imepewa. Kutokana na hali hii ni muhimu kwa daktari kuelewa uhusiano wa kibinafsi na kipekee kati ya wanaume na dhakari zao. Hili litawawezesha kuelewana na wagonjwa wanaume na hivyo kuimarisha mawasiliano nao. Lugha ni muhimu katika utoaji na upokeaji wa huduma za afya. Tabia za lugha ambazo wagonjwa huja nazo hospitalini zinaweza kuathiri mawasiliano kwa njia hasi au chanya. Ni muhimu kuelewa tabia hizi za uhuishi zinazotumiwa na wanaume katika mazungumzo kwa sababu wanataka kuendeleza uhusiano wa kibinafsi na dhakari zao hata hospitalini.

## MAREJELEO

Aceto, M. (2002). Ethnic personal names and multiple identities in Anglophone Caribbean speech communities in Latin America. *Language in Society*, *31*(4), 577-608.

Al-Dilaimy, H., & Thabiti, E. (2017). The Concept of Naming and Definite Descriptions in English and Arabic: A Semantic and Sociolinguistic Analysis. *Journal of Al-Maaref University-College*, 357-377.

Allan, K. (2001). Natural Language Semantics. Oxford: Blackwell.

Cameron, D. (1992). Naming of parts: Gender, culture, and terms for the penis among American college students. *American Speech*, *67*(4), 367-382.

Cornog, M. (1986). Naming Sexual Body Parts: Preliminary Patterns and Implications. *Journal of Sex Research*, *22*(3), 393-398.

Creswell, J. (1998). Qualitative Inquiry and Research Design: Choosing among five traditions. Thousand Oaks,CA: Sage.

Frege, G. (1892). "On Sense and Reference". Translated.

Gacheiya, R. (2018). Peo na Mikakati ya Kimazungumzo katika Uwasilishaji wa Ujinsia

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.685

miongoni mwa Wazulufu. Egerton University: Unpublished PhD Thesis.

Guest, G., Namey, E., & Mitchel, M. (2013). Collecting Qualitative Data: A Field Manual for Applied Research. London: Sage Publications Ltd.

Howlett, B., Rogo, J. E., & Shelton, T. G. (2014). Health-care Research Methods. In B. R. Howlett, Foundations of Evidence-Based Practice for Health Professionals: An Interprofessional Approach. Jones and Barlettt Publishers.

Izugbara, C. O. (2005). Hypothesis on the origin of hegemonic masculinity. *Sexuality in Africa Magazine*, *2*(1), 13-14.

Jayaraman, R. (2005). Personal identity in a globalized world: Cultural roots of Hindu personal names and surnames. *The Journal of Popular Culture*, *38*(3), 476-490. doi:10.1111/j0022-3840.2005.00124.x

Massamba, D. (2004). Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha. Dar es Salaam: TUKI.

Msanjila, Y., Kihore, Y., & Massamba, D. (2009). Isimu Jamii, Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam, Tanzania: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Musyimi, D. (2011). Maana za Majina ya Watu katika Jamii ya Wakamba. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Tasnifu ya Uzamili, Haijachapishwa.

Olatunji, A., Issah, M., Noah, Y., Muhammed, A. Y., & Sulaiman, A. R. (2015). Personal name as a reality of everyday life: Naming dynamics in select African societies. *The journal of Pan African studies*, *8*(3), 72-90.

Ouma, M. (2018). Mitazamo ya Vijana wa Kiume wa Kenya kuhusu Ubabedume: Mkabala wa Uchanganuzi Hakiki Usemi. Egerton University: Unpublished Masters' Thesis.

Potts, A. (2000). The essence of the hard on" hegemonic masculinity and the cultural construction of "Erectile dysfunction. *Men and masculinities*, *3*(1), 85-103. doi:10.1177/1097184x00003001004

Potts, A. (2001). The man with two brains: Hegemonic masculine subjectivity and the discursive construction of the unreasonable penis-self. *Journal of Gender Studies*, *10*(2), 145-156. doi:10.1080/09589230120053274.

Resani, M. (2016). Maana katika Majina ya Wabena nchini Tanzania. Mulika, 35.

Russell, B. (1905). "On Denoting". Retrieved from http://cscs.umich.edu/

Sanders, J. S., & Robinson, W. L. (1979). Talking and not talking about sex: Male and female vocabularies. *Journal of Communication*, *29*(2), 22-30.

Sanders, J. S. (1978). Male and female vocabularies for communicating with a sexual partner. *Journal of Sex Education and Therapy*, *4*(2), 15-19. doi:10.1080/01614576.1978.11074587.

Udechukwu, G. I., & Nnyigide, N. M. (2016). The religious and socio-cultural implication of African names: igbo naming system as a paradigm. *AFRREV IJAH: An International Journal of Arts and Humanities*, *5*(3), 89-103.

Yusuf, N., Olatunji, A. & Issah, M. (2014). Yoruba Names as Reflection of People's Cultural Heritage. In A. A. al (Ed.), Bringing Our Cultures Home Festchrift for Bode Ayayi at 70 (pp. 186-196). University of Ilorin: Department of Linguistics and Nigerian Languages.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.